## WMA YA BURUNGE

WMA ya Burunge ilisajiliwa mwaka 2006 na ilipewa haki ya matumizi mwaka 2007. Ina vijiji tisa[1] wanachama, ambao ni: Kakoi, Olasiti, Magara, Maweni, Manyara, Sangaiwe, Mwada, Ngolei na Vilima Vitatu. Ina takribani ya wakazi 34,000 kutoka makabila ya wambugwe, wabarbaig, wairaqw, wamaasai na Waarusha, ambao chini ya usimamizi wa African Wildlife Foundation na halmashauri ya wilaya walitenga eneo la kilometa za mraba 280 kwa

[illegible]

**Kilelezio Na 4: Jumla ya mapato yaliyorudishwa kwenye WMA ya Burunge (baada ya serikali kukata sehemu yake) na mgawanyo wake kwenye vijiji wanachama kutokea mwaka 2006. Chanzo: Juhibu (2014). Viwango ubadilishaji fedha vimezingatia thamani halisi kwa mwaka husika**

## Mabadiliko ya Hali ya Maisha katika WMA ya Burunge

Watu katika vijiji vya WMA na vile visivyo vya WMA kwa wastani wana kiwango sawa cha ardhi ya kilimo (kwa kipimo cha uwiano wa mtu mzima) (WMA: ekari 1.4 kwa mtu mzima, siyo WMA: ekari 1.5 kwa mtu mzima)

Watu wengi wanayo ardhi zaidi ya kilimo katika mwaka 2014 kuliko waliyokuwanayo mwaka 2007

### Ardhi ya Malisho

Vijiji vyote vya WMA ya Burunge na vile visivyo vya WMA vilikuwa na shida ya upatikanaji wa maeneo ya malisho ya mifugo kwa sasa, kulinganisha na mwaka 2007, isipokuwa kijiji cha Namalulu

Katika vijiji vya WMA upatikanaji wa maeneo ya

**Kielelezo Na. 12: Wastani wa hasara iliyotokana na uharibifu wa mazao kwa kaya katika vijiji vya WMA na visivyo vya WMA. Angalizo: Kiwango cha hasara kimekokotolewa kutokana na makadirio ya eneo lililoharibiwa, uzalishaji wa mazao, na makadirio ya pesa za mauzo ya mazao**

**Kielelezo Na. 13: Kukua kwa idadadi ya wakazi (mraba, mstari wa kulia) na tembo (almasi, mstari wa kushoto). Chanzo: TAWIRI (2014), HDIC (2010), WWF (2014).**

## Hitimisho

Vikwazo katika upatikanaji wa ardhi, maji, kuni na rasilimali nyingine unaathiri wakazi wa WMA ya Burunge. Mifugo, kilimo na mazao ya porini vilichangia robo tatu ya mapato yote ya kaya za WMA na zisizo za WMA kwa mwaka 2014. Kwa wastani, mifugo inayomilikiwa na kaya za WMA na zisizo za WMA ilipungua ikilinganishwa na mwaka 2007. Ardhi ya kilimo haikuwa na mabadiliko tangu mwaka